# Swali La Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy Na Jibu La Imam Muhammad Husain Kashiful Ghitaa wa Najaf

# Swali La Sheikh A. S. Al-Farsy Na Jibu La Imam M.H. Kashiful Ghitaa wa Najaf

Kimetafsiriwa na Sheikh Ramadhan Idris Kwezi

Al-Islam.org

**Publisher(s):**

Bilal Mission of Tanzania [1]

Makala hii inajibu swali la mwanachuoni maarufu wa Afrika Mashariki kuhusu hadhi ya masahaba wa Mtume (s.a.w.w.). Swali limejibiwa na mwenye umahiri wa kielimu na uchamungu wa hali ya juu, aliyeishi katika nchi ya Iraq na aliyehudumia Uislamu na Waislamu kwa zaidi ya miaka 40.

Get PDF [2] Get EPUB [3] Get MOBI [4]

**Translator(s):**

Sheikh Ramadhan Idris Kwezi [5]

# Swali La Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy Na Jibu La Imam Muhammad Husain Kashiful Ghitaa wa Najaf

## Utangulizi

Tunayo furaha kuchapisha barua kutoka kwa Mwanachuoni mashuhuri na maarufu katika Afrika Mashariki Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy, pia tunachapisha jibu la Imam Muhammed Husain Kashiful Ghitaa, mwanachuoni kutoka Iraq anayetambulika kimataifa.

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Sayyid Mohamed Radha mwanae Sayyid Muhammad Mehdi Shushtary mwenye asili ya Zanzibar na ambaye wakati huu anaishi Iran, kwa kuongezea makala zinazowatambulisha Sheikh Adullah Saleh Al-Farsy na Imam Mohammed Husain Kashiful Ghitaa, ambao wanajulikana vema ulimwenguni kote. Hii ni kwa manufaa ya kizazi kipya ambao pengine watakuwa hawajui wao.

Pia tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Masheikh Haroun R. Pingili na Musabah Sha'aban, kwa msaada wao wa kupitia kitabu hiki na kutoa maoni yao ambayo yamewezesha kufanikisha kitabu chote.

**Wabillah Tawfiq,**
**Bilal Muslim Mission of Tanzania**

# 1. Ni Nani Sheikh Abdullah Saleh Farsy?

Marehemu Sheikh Abdullah Saleh Farsy alizaliwa mjini Zanzibar mnamo February 1912.

Alikuwa miongoni mwa Maulamaa wakubwa katika nchi za Afrika ya Mashariki na ya kati, na alikuwa ni miogoni mwa Wanavyuoni wachache waliozitawala fani mbili za uandishi na ukhatibu. Ni Mwanachuoni aliyejizatiti kwa elimu za kisekula na kidini, na kwa wakati huo huo hakuwa mgeni katika fani ya ushairi.

Alimaliza masomo yake ya Ualimu katika Teachers' Trainning School mwishoni mwa mwaka 1932. Baada ya kufaulu vizuri kabisa daraja la mwanzo katika masomo yake, akaanza kufanya kazi ya Ualimu katika shule za serikali za Unguja kuanzia mwaka 1933 hadi 1947. Kisha akapandishwa cheo na Serikali ya Zanzibar na kuwa Mkaguzi wa mambo ya dini na lugha ya kiarabu katika skuli za serikali, tangu mwaka 1949 hadi 1952 (barua hii alimwandikia Ayatullah Kashiful Ghitaa alipokuwa mwaka wa mwisho wa ukaguzi wake)

Kuanzia mwaka 1952 hadi 1954, Sheikh Farsy alishika wadhifa kama Mwalimu Mkuu wa chuo cha Dini cha Muslim Academy cha Zanzibar, chuo ambacho kina fakhari ya kuwafunza Masheikh, Makadhi wa walimu wengi kutoka sehemu mbaimbali za Mashariki mwa Afrika.

Katika kipindi cha mwaka 1954-1956, aliwasomesha ualimu, walimu wa Refresher Course: na akawa mwalimu mkuu wa shule katika kipindi cha mwaka 1957-1958. Mnamo mwaka 1959, akawa mwalimu katika Teachers' Training College.

Umaarufu wake katika elimu za Kiislamu na huduma zake katika jamii ya Kiislamu, uwepesi wake wa kuchangamana na wafuasi wa madhehebu mbalimbali ya Kiislamu, na ubashasha wake kwa wazee hadi watoto, vyote hivyo vilichangia katika kumpatia umashuhuri na kumpelekea kuteuliwa kuwa kadhi Mkuu wa Zanzibar tangu mwaka 1960 hadi 1967.

Baada ya kutoa huduma zake kwa Serikali ya Zanzibar kwa zaidi ya miaka 30, Sheikh Abdallah Saleh Farsy alihamia nchini Kenya ambapo akateuliwa kuwa Kadhi Mkuu (chief kadhi) wa Kenya nzima katika mwaka 1968 baada ya kustaafu aliyekuwa kadhi Mkuu, marehemu Sheikh Muhammad Kassim al-Mazrui, ambaye alikuwa sahibu wake wa chanda na pete. Mnamo tarehe 28 Februari 1981 alitunukiwa wadhifa mwingine na Serikali ya Kenya na kuwa Hakimu Mtembezi wa taasisi zote za Mahakama za jimbo la Pwani la Kenya. Baada ya kutoa huduma zake kwa Serikali na Waislamu wa Kenya kwa miaka 13, alilazimika kustaafu kwa sababu ya uzee, afya na mambo ya wanawe, na akahamia Maskati katika Usultani wa Oman ambapo alifariki dunia siku ya Jumatatu tarehe 8 Novemba 1982.

Sheikh Abdullah Saleh Farsy amesoma masomo yake ya dini kutoka kwa Mashekhe mbalimbali wa Zanzibar na wengine kutoka nje na kwa kadiri fulani, hata kutoka kwa Maulamaa wa kishia. Alisoma kutoka kwa Sheikh Abdul Baariy al-Ajizy kutoka al-Azhar (Misri) na mashekhe mbalimbali wa kishia waliokuwa wakitembelea Zanzibar ambapo masahibu wa Kishia wa Sheikh Farsy walimkutanisha na

kufanya Jalasa za kielimu kuhusu madhehebu ya Ahlul Bayt.

Mashekhe wengine waliomsomesha Sheikh Farsy waliokuwa: Sheikh Ahmed Muhammad Mlomry Commorian (f. 1357 H), Sheikh Abubakar bin Abdalla Bakathir (f.1943 M), Sheikh Muhammed bin Abdul Rahman Makhzumy (f. 1946 M), n. k.

Lakini utafutaji wa elimu wa Sheik Abdullah Saleh haukukomea katika darsa za Masheikh peke yake, bali alionyesha kiu yake ya kujielimisha kwa kusoma vitabu vingi , vikiwemo vya madhebu ya Kishia, kwa kuandikiana na Maulamaa wakubwa wa Kishia waliokuwepo katika nchi za Lebanon na Iraq, India na Pakistan. Kwa sababu hii, tunamwona Sheikh Farsy akiwa na mahusiano mazuri na viongozi na wafuasi wa madhehebu yote ya Kiislamu. Na haya yanadhihirika katika tafsiri yake, vitabu, khutba na mazungumzo yake.

Sheikh Farsy ameandika zaidi ya vitabu mia kwa lugha ya Kiswahili, na vichache kwa lugha ya Kiarabu. Yeye ni miongoni mwa Maulamaa wachache wa Afrika Mashariki waliotajirisha Umma wa Kiislamu wa Afrika Mashariki kwa Vitabu na Khutba zake, Tafsiri ya kiswahili ya Qur'ani Takakifu imechukua nafasi ya pekee na ya juu kabisa. Kuhusu tafsiri hiyo, mwanafunzi wake, Sheikh Saidi Musa, ameandika haya: Fikra zake Sheikh kuhusu kuifasiri Qur'ani Tukufu, zilimjia tangu alipoanza kutunga vitabu vya dini kwa lugha ya kiswahili mnamo mwaka 1942 alipokitoa kile kitabu cha maisha ya Nabii Muhammad (s.a.w.w) na alianza kutafsiri Qur'ani Tukufu kabla ya mwaka 1949.

Mnamo mwaka 1949 akawafikiwa kuchapisha Sura za sala na tafsiri zake, akiwa na maana kuwa ataendelea kuchapisha tafsiri yote nzima (kumalizika). Kwa taabu ya kuchapisha, tafsiri yake ilichelewa kutoka na ikatoka kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 1969 akiwa huko Mombasa, Kenya." Taz (Bid-a, jz 2, uk. ix-x).

Kwa upande wa kutoa mawaidha ya kidini, mbali na darsa zake misikitini, mawaidha yake katika idhaa ya Unguja yalikuwa maarufu na yakisikilizwa na Waislamu katika Afrika Mashariki nzima. Alikuwa akitoa mawaidha katika Idhaa ya Unguja mara nyingi kila siku, tangu alipohamia mpaka alipohama.

Miongoni mwa huduma nyingi za Kiislamu zilizotolewa na Sheikh Farsy – mbali na vitabu na mawaidha – ni kuwafunza Walimu na Masheikh wengi ambao wametawanyika katika sehemu mbalimbali za Afrika ya Mashariki na hata Ulaya na Uarabuni. Mambo hayo yote ndiyo yaliyompelekea marehemu Sheikh Abdullah Saleh Farsy kutambuliwa na kuheshimiwa hata Mashariki ya kati kama ni mwanachuoni mkubwa wa Kiislamu.

## 2. Ni Nani Ayatullah Muhammad Husain Kashiful Ghitaa?

Marehemu Ayatullah Muhammad Husain Kashiful Ghitaa alizaliwa katika Mji mtakatifu wa Najaf (Iraq) katika mwaka 1294 Hijria (1876 Miladia). Alipata malezi na mafundisho ya Kiislamu katika ukoo wa Aali Kashiful Ghitaa ambao ulisifiwa kwa kutoa wanavyuoni wakubwa kwa ajili ya Umma wa Kiislamu, na

kwa harakati zao za kidini katika kipindi cha miaka 180 tangu babu yake Sheikh Khizr bin Yahya alipohamia mjini Najaf. Alipokuwa na umri wa miaka sita tu, kipawa cha werevu wake kilianza kubainika kati ya wanavyuoni wa Iraq ambapo alikuwa akihudhuria na kushiriki katika darsa na majlisi mbalimbali pamoja na baba yake.

Alipokuwa na umri wa miaka 15 tu, aliandika kitabu chake cha kwanza kuhusu ukoo wa Kashiful Ghitaa, na kwa njia hiyo kuwapa mshangao mashekhe wake na wanafunzi wenzake. Alimaliza masomo yake ya kimsingi katika lugha ya kiarabu, fikihi na usuli akiwa na umri mdogo bado. Akaendelea kwa shauku na juhudi katika masomo ya kiwango cha juu katika Chuo cha kidini (Hawza) cha Najaf kwa kuhudhuria darsa na mihadhara ya wanavyuoni wakubwa wa zama hizo. Miongoni mwa masheikh wake walikuwa:Ayatullah Mustafa Tabrizi, Ayatullah Mirza Muhammad Baqir Istihbanati, Ayatullah Ahmad Shirazi, Ayatullah Muhammad Ridha Najafabadi, n.k.

Kipawa cha elimu cha Ayatullah Kashiful Ghitaa kilikuwa kikubwa mno kwa kadiri kwamba aliweza kuzitawala elimu zote zilizosomeshwa chuoni humo katika muda mfupi hali akiwa kijana kabisa. Kwa sababu hiyo, alitumainiwa na kutegemewa na maulamaa wa Hawza ya Najaf na hasa mujtahid na marja'–taklidi (Mufti Mkuu) wa zama hizo, Ayatullah Sayyid Muhammad Kadhim Yazdi ambaye alimpa kazi ya kujibu Masuala ya kidini.

Baada ya kufariki Ayatullah Yazdi, Waislamu wengi wa Iraq walimkalidi Ayatullah Kashiful Ghitaa kama ni marja' na kiongozi wao. Mihadhara na darsa zake zilikuwa zikihudhuriwa na wanafunzi wengi wa kidini kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu wa Kiislamu ambao walizikusanya darsa zake na kuzichapisha katika majalada mengi.

Khutba zake zilikuwa tamu, zenye kuathiri na kuhamasisha, na zilikuwa na jazba maalum kwa kadiri kwamba wasikilizaji hawakuchoshwa hata kama aliendelea kukhutubu kwa muda mrefu.

Vyuo vya Kiislamu katika Miji ya Najaf, Baghdad, Cairo, Quds, Tehran na Karachi havijasahau mihadhara yake iliyokuwa ikivuma.

Ayatullah Kashiful Ghitaa mbali na umahiri wake wa kielimu na uchamungu wake wa hali ya juu, alikuwa mwanachuoni mkakamavu, mwanaharakati na mwenye fikra pana – hivyo, aliweza kuwavutia maulamaa na maamuma na kuingiliana nao kwa urahisi.

Alikuwa msafiri mzuri. Alizitembelea nchi kadhaa za Kiislamu ambako alikutana na wanavyuoni wa madhehebu mbalimbali ya Kiislamu na kujadiliana nao juu ya masuala kadhaa ya kielimu, na kuwatanabahisha juu ya njama za wakoloni. Ilikuwa ni kawaida yake kila alipofika katika mji mmoja, alikaa hapa kwa muda siku kadhaa au kwa miezi kadhaa kwa shabaha ya: kubadilishana fikra na Maulamaa mbalimbali, kuzungumzia masuala ya kidini, kuwazindua wakazi wa hapo juu ya njama za wakoloni dhidi ya Uislamu na Waislamu, kusimamia uchapishaji wa vitabu vyake, n.k.

Alikaa zaidi ya miezi sita katika mji wa Cairo ambapo alikuwa na wanavyuoni wa kidini na wahadhiri wa

Chuo Kikuu cha Al-Azhar.

Vivyo hivyo, alionana na wanafunzi wa al-Azhar na akawaanndalia semina, na hata alitoa khutba za kuvutia sana katika baadhi ya Makanisa ambapo alibainisha makosa ya wamisionari wa Kikristo.

Ayatullah Kashiful Ghitaa alithibitisha ukakamavu na mwamko wake kutokana na harakati zake za kisiasa dhidi ya udhalimu na ukoloni katika nchi za Kiislamu. Katika mihadhara na vitabu vyake, alisisitiza sana juu ya umoja wa Waislamu unaoleta faida kwa maadui, na aliwanasihi wawe kitu kimoja katika msimamo wao dhidi ya dhulma.

Mnamo mwaka 1350 Hijria, alikwenda Palestina kushiriki katika mkutano wa Muutamar Al- Islami uliofanyika Mjini Quds. Katika mkutano huo, shakhsia mbalimbali kutoka nchi za Kiislamu, wakiwemo Rashid Ridhaa (mwanafunzi wa Sayyid Jamaluddin Assadabadi), na Allamah Iqbal Lahori. Karibu Waislamu sabini elfu kutoka kila pembe ya Palestina walishiriki katika mkutano huo na wakasali nyuma yake katika Msikiti wa (Masjid) Al- Aqsa.

Alitoa hotuba muhimu na ya kihistoria katika mkutano huo ambayo iliwavutia sana washirika wa mkutano huo. Alizungumzia masuala muhimu yaliyokuwa yakiukumba ulimwengu wa Kiisalamu na jinsi wakoloni walivyokuwa wakila njama zao za hatari dhidi ya ulimwengu wa Kiislamu. Alibainisha maana halisi ya umoja kati ya Waislamu na akawataka washikamane na Qur'ani Tukufu na Sunna za Mtume Muhammad (s.a.w) katika kutekeleza umoja huo miongoni mwao.

Hotuba hiyo kali ya Ayatullah Kashiful Ghitaa ilichapishwa katika magazeti na kuenezwa ulimwenguni kote. Wanafikra na waandishi wengi wa Kisunni ambao walikuwa na mtazamo mbaya kuhusiana na Ushia, walirekebisha fikra zao baada ya hotuba hiyo. Baada ya kusikia hotuba hiyo ya Mwanachuoni mkubwa wa kishia, walitambua kwamba walikuwa wakiwadhania vibaya ndugu zao wa kishia kutokana na kuathiriwa na fikra mbaya na propaganda zenye sumu zilizokuwa zikienezwa na wafatini na maadui wa Uislamu. Umashuhuri wake ulizidi baada ya mkutano huo wa Palestina na akaanza kuitwa kama kiongozi.

Katika mwaka 1371 Hijria, alikwenda mjini Karachi kuhudhuria Mkutano wa Kiislamu ambapo alikuwa mgeni rasmi wa serikali. Alitoa hotuba kali na za hamasa kuhusu hali ya kijamii na kisiasa ya nchi za Kiislamu.

Vita vya Kwanza vya Dunia vilioanza, Ayatullah Kashiful Ghitaa alikuwepo nchini Lebanon. Aliondoka haraka kwenda kushiriki katika mapambano ya wananchi wa Iraq dhidi ya majeshi ya wavamizi wa Uingereza, na akavaa nguo za kijeshi na kuchukua bunduki. Yeye pamoja na mujtahidi wengine, walitoa fatwa ya jihadi dhidi ya Mwingereza. Aidha alishiriki kwa ushujaa na ujasiri mkubwa katika mstari wa mbele katika mapambano ya watu wa Najaf dhidi ya majeshi ya Uingereza.

Alipoalikwa katika Mkutano wa Bihamadun uliofanywa na waunga mkono wa ukoloni wa Marekani, si tu kwamba aliukataa mwaliko huo, bali aliandika kitabu kimoja kufichua njama na malengo ya mkutano

huu. Kitabu hicho kinaitwa: *al- Muthul al "Ulyaa fil Islam laa fii Bihamadun* (*Mifano bora katika Uislamu si katika Bihamadun*).

Alikuwa ni mwandishi wa vitabu aliyefanikiwa mno kutokana na uandishi wake katika masuala mbalimbali ya kielimu, kidini, kifiqihi, kiitikadi, n.k.Ametunga zaidi ya vitabu 30.

Baada ya kuuhudumia Uislamu na Waislamu kwa zaidi ya miaka 40, Ayatullah Sheikh Muhamad Husain Kashiful Ghitaa alifariki dunia nchini Iraq siku ya jumatatu tarehe 18 Dhilqaad 1373 na akazikwa mjini Najaf karibu na kaburi la Amirul Mu'uminiin Ali bin Abu Talib a.s.

## 3. Barua ya Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy

Akiuliza swali lake
3 jamadil Awwal, 1373 Hijria (1952)

*Assalaamu alaikum wa rahmatullahi wa barakatuhu.*

Amma baada ya salamu, Mimi ni mfuasi wa madhehebu ya shafii, ambaye ni rafiki mpenzi wa baadhi ya (Mashia) Ithnaasharia halisi. Wakati mwingine tumekuwa tukijadiliana kuhusiana na tofauti za kimadhehebu. Nao (Mashia) wamenieleza kuwa masahaba wakubwa: Abu Bakr, Umar, Uthman, pamoja na masahaba wengine, wote wakiwa kumi, ambao wamebashiriwa kuingia peponi, nyinyi mnaamini kwamba wao ni watu wa Motoni.

Je, hilo linawezekana baada ya Mwenyezi Mungu kusema katika kitabu chake kitukufu (Qur ani) kuwa:

***Na wale waliotangulia wakawa wa kwanza katika*** **(*Uislamu*)** ***– Muhajirina na Ansari, na wale waliowafuata kwa mwendo mzuri – Mwenyezi Mungu atawapa radhi, nao wamridhie*** **(*Mwenyezi Mungu kwa hayo mazuri atakayowapa*)** ***na amewaandalia Mabustani yapitayo mito mbele yake, wakakae humo milelee. Huku ndiko kufuzu kukubwa. "*** **(*at-Tawbah, 9:100*)**

Je, hao si wale waliotangulia wakawa wa kwanza katika Muhajirina? Je, Aya hiyo haiwahusu watu hao?

Naye Sayyidna Umar bin Khattab ni miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu amesema kuhusiana nao (hivi):

***"Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewapa radhi Waislamu walipofungamana nawe chini ya mti: na alijua yaliyomo nyoyoni mwao..."*** **(*al-Fath, 48:18*)**

Vilevile (Mashia hao) wamenieleza kwamba wanawalaani masahaba wengi, badala ya kuwaombea rehema hivyo ndiyo inavyostahiki kuwafanyia Masahaba wetu? Je, Mwenyezi Mungu hakuwagawa waumini katika daraja tatu- Muhajirina, Ansari, na wale waliokuja baada yao? Na Mwenyezi Mungu amewasifu kwa wao wanasema:

***" Mola wetu! Tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia*** (***kufa***) ***katika Imani. wala Usiweke mfundo katika mioyo yetu kwa walioamini; Mola wetu! Hakika wewe ni mpole sana, Mwenye rehema mno."*** (***al-Hashr, 59:10***)

Mwenyezi Mungu hakuwasifu (masahaba hao) kwa vile wanasema: "Mola wetu!Mlaani Fulani na Fulani, na usiondoshe chuki ndani ya nyoyo zetu!"

Ni matarajio yangu makubwa yanayotokana na hadhi yenu kubwa na elimu yenu safi, kuwa hamtafanya ubakhili katika kunijibu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

***Hakika wale wanaoficha tuliyoyateremsha nazo ni hoja zetu zilizo wazi na uwongofu baada ya sisi kuzibainisha kwa watu kitabuni - hao anawalaani Mwenyezi Mungu, na wanawalaani*** (***kila***) ***wenye kulaani."*** (***al- Baqarah, 2:159***)

Tunamwomba Mwenyezi Mungu muendelee kuwa kiigizo na makimbilio ya elimu. Na Imam (Ali) amesema kweli, na ataendelea kuwa mkweli, na mwenye kusadikika kutokana na maneno yake yafuatayo:

Ni fakhari Yao kweli, pekee kwa wenye elimu, kutoa zao dalili, hakika wameongoka.

Mtumwa wenu,
Abdullah Saleh Al-Farsy
Mkagizi wa Mambo ya Dini Lugha ya Kiarabu katika
Skuli za Serikali.

## Majibu ya Imam Muhammad Husain Kashiful Ghitaa

Nimepokea barua yako tukufu ambayo unaeleza kuwa wewe ni mfuasi wa madhehebu ya Shafii, na kwamba ni rafiki mpenzi wa baadhi ya Mashia Ithnasheria halisi, na kwamba wao wamekueleza kuwa masahaba wakubwa, pamoja na wengine, (wote wakiwa kumi) ambao walibashiriwa kuingia Peponi, wataingia Motoni kulingana na imani yetu. (Shia ithnaashari).

Baadaye ukauliza: Je, hilo linawezekana baada ya Mwenyezi Mungu kusema:

***"Na wala waliotangulia wakawa wa kwanza katika*** (***Uislamu***) ***Muhajirina na Ansari, na wale waliofuata kwa mwendo mzuri – Mwenyezi Mungu atawapa radhi, nao wamridhie..." hadi mwisho wa aya.***

Tena ukasema: Je, inawezekana kwa watu hao kuritadi na kuurejea ukafiri wao hali Mwenyezi Mungu amekwishawaridhia baada ya kuyajua yaliyo nyoyoni mwao? Je, elimu ya Mwenyezi Mungu inaweza kugeuka na kuwa ujinga? Tena ukasema katika jambo hilo kuwa (Mashia) wanawalaani masahaba wengi badala ya kuwaombea rehema. Na umehitimisha barua yako kwa kusema, "ni matarajio yangu

makubwa yanayotokana na hadhi yenu kubwa na elimu yenu safi kuwa hamtafanya ubakhili katika kunijibu."

Ukamaliza barua yako yenye kupendeza kwa kunukuu Aya bainifu (za Qur'ani Tukufu) na maneno matamu.

Kwanza kabisa, elewa na uwe na yakini kwamba (Mashia) Ithnasheria wenye akili na wenye adabu si watu wenye kulaani na hawana tabia ya kutukana, kwani Maimamu wetu wa Ahlul Bayt (amani iwe juu yao) wametukataza kulaani na kutukana. Hivyo, sisi hatuwalaani wala hatuwatukani makhalifa waongofu na masahaba walioridhiwa ambao Mwenyezi Mungu amewaridhia, nao wakawa radhi naye.

Pamoja na hayo, hatuna budi katika kukujibu tukufunulie ufuniko uliofunika ukweli halisi na kukueleza hali halisi ilivyo. Pia ni lazima tukufahamishe waziwazi, japo kwa sura ya ujumla na udokezo, kwani hakuna shaka kuwa wewe ni mtu huru (mwenye kuwa na fikra pana).

Ukweli ambao huwezi kuukataa wala hatuna shaka kuwa wewe unaujua na ni lazima uukubali na kuukiri ni huu: kwamba kwa hakika si masahaba wote waliosuhubiana na Mtume (s.a.w.w) miongoni mwa muhajirina wote walioridhiwa na Allah, wala si wote wanajumuika katika kauli yake Mwenyezi inayosema;

***Mwenyezi Mungu ameridhika nao, nao wameridhika naye."***(***9:100***) wala si masahaba wote wanaoingia katika ***"ndugu zetu waliotutangulia:"*** (***59:10***)

Kwani Qur'ani Tukufu inajifasiri yenyewe kwa yenyewe na hujithibitisha yenyewe kwa yenyewe.

Hivyo, inalazimika kuziunganisha na kuzihusisha baadhi ya Aya na Aya nyinginezo ili ukweli uweze kudhihirika ukiwa mweupe wenye kung'ara kabisa.

Na kama masahaba wote wangekuwa ni wenye kuridhiwa kwa vile ***"Mwenyezi Mungu ameridhika nao, nao wameridhika naye"***, basi maneno haya ya Mwenyezi Mungu yatakuwa na maana gani?

***Na hakuwa Muhammad ila ni Mtume tu.Wamepita kabla yake Mitume*** (***wengi kabisa***)***. Je, Akifa au akauwawa ndiyo mtarudi nyuma*** (***kwa visigino vyenu***)***,.... muwe makafiri kama zamani?"*** (***Aaali-Imran, 3:144***)

Ingekuwa vizuri kama tutawajua watu hao. Je, inawezekana kuwajua ni nani hao waliotaka kugeuka na kurudi nyuma? Ni jambo lililo wazi kuwa uulizaji (Istifhaam) katika Aya hiyo ni ya kukemea (inkaari). Na maana yake ni hii kwamba – jambo fulani hufanywa na mmoja au watu kadhaa ambapo mwenye kusema hukemea (jambo hilo) kwa namna ya kuuliza. Na maana ya kukemea kwake huko ni dalili inayoonyesha kwamba jambo hilo limekataliwa na ni baya.

Ninapenda kukuzidisha faida na kuwekea mambo wazi, kwa kukupa dalili ili kukuondolea utata uliokupata, ni kwamba: kama ilivyo Qur'ani Tukufu inajifasiri yenyewe kwa yenyewe. Hivyo hivyo sunna

za Mtume na hadithi zinaifasiri Qur'ani Tukufu na kuifafanua.

Tazama kitabu "Sahih Bukhari" ambacho ni kitabu sahihi kabisa cha hadithi kwa Waislamu wa madhehebu ya Shafii na wasiokua Shafii miongoni mwa madhehebu manne ya Kisunni. Hakika wewe utakuta ndani yake na ndani ya kitabu kingine cha hadithi kiitwacho "Sahih Muslim" hadithi zenye miundo mbalimbali, lakini zenye maana moja, na zenyewe. Miongoni mwa hadithi hizo ni hii:

Amesema Mtume (s.a.w.w):
"Mimi nitawatangulia kufika kwenye hodhi (birika la maji) na wanaume miongoni mwenu watanikimbilia lakini hawatanifikia. Nitasema: Ewe Mwenyezi Mungu! Masahaba wangu! Na nitaambiwa:

"Hakika wewe hujui waliyoyazusha baada yako". Basi itatolewa amri waingizwe Motoni. Nami nitasema: Maangamio! Maangamio!~ Ni kwa wale walioyageuza na kuyabadilisha mafunzo ya Uislamu baada yangu."

Na Mtume anasema katika hadithi nyingine ambayo maneno yake au madhumuni yake yana maana yafuatayo:
"Kikundi cha masahaba wangu kitaamriwa kuingia Motoni. Nitasema: kwa nini wanaingizwa Motoni?" Nitaambiwa: Hakika wao waliritadi kwa kuurejea ukafiri."

Haya ni machache tu ambayo nimekuandikia miongoni mwa kumbukumbu zangu nilizopitia nakuzihifadhi, kiasi cha miaka hamsini iliyopita. Na kwa wakati huu sina muda kufanya marejeo mapya. Kwa hivyo, wewe mwenyewe kama unataka, fanya marejeo sawasawa, hadi mambo yawe waziwazi kwako. Nawe utafahamu kuwa sio masahaba wote waliopata radhi ya Mwenyezi Mungu na wao wakawa radhi naye pia.

Vilevile utafahamu kuwa watu wengi zaidi waliritadi baada ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na wakayarejelea ya kale (ukafiri). Haya tunayasema kwa ushahidi wa Aya za Qur'ani Tukufu na hadithi za Mtume (s.a.w.w) kutoka ndani ya vitabu vyenu wenyewe na wala sio vitabu vya Shia Ithnasheria.

Ninakumbuka kuwa ninazo zaidi ya hadithi ishirini (20) kutoka katika Sahihi Bukhari na Sahihi Muslim. Zenye sanadi nyingi na ibara tofauti tofauti, zote zikieleza waziwazi kuwa masahaba wengi baada ya Mtume Muhammad (s.a.w.w) waligeuza na kubadilisha imani zao na wakarejea ujahili wao wa mwanzo, na wala Mwenyezi Mungu hakuwaridhia na wao hawakupata radhi zake. Walimkasirisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa amali zao (mbaya). Haya niliyokuambia yatazame ndani ya sahihi mbili tutakuandikia mwisho wa barua yetu hii, riwaya halisi na hadithi zilizoelezea hali ya masahaba, ndani ya sahihi mbili na utayakuta yakiwa dhahiri tena wazi.

Hebu tujaribu kufumbia macho kitabu na Sunna, pamoja na dalili zake zilizo wazi, na sasa tuzigeukie hisia na hali halisi, kwani ni ushahidi na hoja yenye nguvu. Na hebu turejee kwenye tukio lililotokea na mkasa ulio mashuhuri kabisa, Je! umeona kama ukiwakuta watu wawili wanagombana juu ya jambo fulani, na ugomvi huo ukawafikisha mahala ambapo kila mmoja wao anataka kumuua mwenzake, Je!

Kwa akili yako unaona kuwa kuna nafasi ya kuhukumu kuwa wote wana haki? yaani haki ipo kwenye pande zote mbili sambamba, zilizopingana katika mwelekeo na uvutano, "sivyo kabisa:" Haki haipingani. Na muelekeo na mvutano ni vitu viwili vinavyopingana. Na vitu viwili vinavyopingana havikutani na havinyanyuki.

Je, Khalifa Uthuman bin Affan hakuwa ni katika masahaba waliojitokeza msitari wa mbele na Muhajirina wa kwanza? Je, watu wa Madina hawakujumuika katika kumwua? Na wote au wengi wao hawakuwa ni masahaba walau kwa dharura? Na pamoja nao walikuwemo watu mbalimbali kutoka nchi za Kiislamu, baadaye walimuua Khalifa Uthuman kifo kibaya, wakati katika hadithi mashuhuri, Mtume (s.a.w.w) amesema:

"Si halali kumwua Mwislamu ila kwa moja kati ya hayo mambo matatu:

1) Kuritadi kwenye imani
2)Au zinaa katika ndoa
3)Au kisasi kwa kuua nafsi iliyoharamishwa kuuawa."

Mimi sijui ni lipi mojawapo kati ya hayo matatu waliohalalisha tendo la kumuuwa Khalifa. Na labda watu wa Madina ndio wajuzi wa hayo.

Halafu tumtazame Talha na Zubair ambao ni miongoni mwa masahaba maalumu wa Mtume Muhammad (s.a.w.w), na ni katika Mujahidina wa mwanzo na Muhajirina wa kwanza kabisa. Na upanga wa Zubair ndio upanga ambao mara nyingi uliondoa taabu na shida mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Je! masahaba hawa wawili hawakusimama dhidi ya kiongozi wa waumini Sayyidna Ali (a.s) na kumhadaa Mwanamke masikini Bibi Aisha, Mama wa Waumini, ambaye alipanda ngamia na baadaye nyumbu?

Hao masahaba wawili waliuawa katika vita vya kuangamiza, na wasingeuana ila kwa sababu ya kumwendea kinyume na kumfanyia jeuri Imamu wa wakati wao, ambaye walikula kiapo cha kumtii, lakini baadaye wakavunja nyumba yake kumfanyia ujeuri.Wasingeuawa ila baada ya kuuwa (katika vita vile) zaidi ya watu elfu kumi kwa uchache!

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema katika Qur'ani Tukufu:

***"Na ikiwa makundi mawili katika Waislamu yanapigana, basi fanyeni suluhu baina yao na likiwa moja ya hayo linamdhulumu mwewnziwe basi lipigeni lile linaloonea..." (al – Hujuraat, 49:9).***

Mimi sielewi: Hivi kweli Talha na Zubair (r.a) wao ni miongoni mwa wale ambao Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alilalamika na kusikitika kwa kusema:

*"Nitaliona kundi la masahaba wangu wanapelekwa Motoni, ni nitasema: "Mungu wangu masahaba wangu! Masahaba wangu! Na nitaambiwa: Wewe huyajui waliyoyafanya baada yako,hakika wao walirejea kinyume nyuma na wakaritadi baada yako."*

Amma Muawiyah ambaye mnamhesabu kuwa ni miongoni mwa maswahaba pamoja na kuwa kamfanyia jeuri kiongozi wa Waumini, Sayyidna Ali (a.s) katika vita vya Siffin ambavyo waliuawa zaidi ya Waislamu ishirini elfu kutoka pande zote mbili kulingana na ninavyoona mimi, sivijumuishi katika idadi ya yale matukio maalum, kwa sababu Muawiyah na baba yake (Abu Sufyan) na Al-Hakam na mwanawe Marwan, hawakusilimu na hawakumwamini Mwenyezi Mungu hata kwa kiasi cha kufumba na kufumbua jicho, sio kabla ya kuikomboa Makka. Na kwa kweli walijidai tu kuwa ni Waislamu.

Muawiyah bin Abu Sufyan katika vita vya Siffin aliwauwa watu bora kabisa miongoni mwa masahaba Waislamu, kwa mfano Bwana Amru bin Hamq[1] na Hajar bin Adiy[2] na masahaba wengine kumi amewauwa kwa dhuluma na uadui.

Miongoni mwa mambo machafu ya Muawiyah ni kumpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na kuwauwa maraihani wawili wa Mtume, Hasan na Husain. Na kuna mambo mengi mengine machafu ya Muawiyah hayana idadi wala kikomo.

Hivyo Muawiyah bin Abu Sufyan mnamfanya kuwa ni sahaba wa Mtume, na ni miongoni mwa wale ambao wamepata radhi za Mwenyezi Mungu.

Na kama huo ndio Uislamu, basi Uislamu wenyewe tunausomea Fatiha kwani kubakia katika ukafiri ni bora kuliko Uislamu huo wa Muawiyah bin Abu Sufyan, Hakam, Marwan na Wazagh bin Wazagh kama alivyosema Mtume (s.a.w.w). Kwa ujumla sina shaka tena na wala sidhani iwapo kuna kitu kingine cha kuongeza ila ni kwamba: Haki imeshadhihiri mbele yako, na jua la ukweli wa mambo limeshachomoza juu yako, na fumbo linakolea zaidi kuliko maneno.

Mwenyezi Mungu na Waislamu wanashuhudia kuwa ninachukia sana kuongea sana haya mambo yanayosumbua, ambao yanachemsha mambo yaliyokwishapita siku nyingi na kusahaulika; na yanayaeneza chuki ndani ya vifua vya makundi ya Waislamu. Lakini kutokana na kusisitiza kwako, kutaka jawabu, ndiko kulikonipelekea kutoa haya maneno kwa mtiririko wa kalamu, na huku nikiwa ni mwenye kukereheka.

Na hiyo siyo mipango yangu na hatua zangu, kwani mimi tangu miaka hamsini iliyopita, ninapigania kukusanya na kuunganisha umoja wa neno la Waislamu, na kuondosha ubinafsi, ukiritimba na chuki, miongoni mwa Waislamu, na badala yake tushikamane na kamba imara ya Mwenyezi Mungu kwa upole na Mapenzi bila mtafaruku na utengano.

Na tuushike udugu wa Waislamu ambao umefungwa ndani ya Qur'ani Tukufu. Mwenyezi Mungu amesema: ***"Hakika waumini ni ndugu***." (***al – Hujuraat, 49:10***).
"Na ushahidi wa hayo utaupata ndani ya vitabu vyangu nilivyovitunga kwa mfano:Utangulizi wa kitabu kiitwacho *"Aslu"sh-shi"ah wa Usuliha"* kitabu ambacho kimechapwa mfululizo mara kumi, na kimefasiriwa katika lugha mbalimbali, na vitabu vinginevyo.

Umenibana na umenitishia kwa kuniandikia Aya ya Qur'ani Tukufu, ambayo Mwenyezi Mungu anasema:

***“Hakika wale wanaoficha yale tuliyoyateremsha nazo ni hoja zetu zilizo wazi na uwongofu baada ya sisi kuzibainisha kwa watu kitabuni - hao anawalaani Mwenyezi Mungu, na wanawalaani*** (***kila***) ***wenye kulaani.”*** (***al – Baqarah 2:159***).

Na mimi sikupata njia yoyote ya kuondoka na uwajibikaji katika jambo hili zaidi ya hivi nilivyofanya kwa kueleza kiasi Fulani cha matukio.
Kama yote hayatakuwa ni sahihi, lakini angalau kwa kiasi fulani sehemu ya ukweli huo umetajwa. Na inawezekana kabisa sehemu hiyo ikatoa mwangaza mkubwa kuhusiana na yote yanayoelekea kwenye tukio hilo. Na ninamalizia barua yangu kwa maneno mafupi ya babu yangu mpenzi ***Sheikh Mkuu Bwana Jaafar***, mtungaji wa kitabu *Kashiful Ghitaa*.Yeye anasema katika kuhitimisha maneno haya:
“Zitazame hali za watu na uziweke mbele yako kwa uchunguzi zaidi, na ukiwa umezikodolea macho yako mawili, na huku ukitia fikra katika matawi na matukio, ili uweze kujua hali za asili (yake) na kumaliza ugomvi. Kwa njia hii unaweza ukaitazama Basra, nayo ikakuonyesha; na vita vya ngamia vinaweza kukupa onyo na vita vya ngamia vinaweza kukusafishia (njia) nayo ni Karbala na (mji wa) Kufa utakutosha (kuzingatia).”

Kutofautiana katika maelezo yenye ushahidi na kuwepo migongano katika pande mbili ni ushahidi tosha kabisa kuwa haki ipo kwenye upande mmoja wa mzozo; na kweli, kutoa uamuzi kwamba pande zote mbili zina haki, ni itikadi mbovu.

***“Hakika wewe huwezi kumwongoza umtakaye lakini Mwenyezi Mungu Humwongoza amtakaye..*** (***Al-Qasas,28:56***)
“Utakasifu ni Wako, ***“Mungu wetu, sisi tunaweka mategemeo yetu juu yako, na kwako twatarajia, na kwako ndiko kuna marejea.*** (***Al-Mumtahana 60:4***)

**7 Rajab 1373 Hijri**
**Katika Chuo chetu cha kidini**
**(Najaf, Iraq)**

1. Amr Ibn Al-Hamiq Al -Khuzai, ni sahaba mtukufu mno na muaminifu, yeye ni miongoni mwa wandani wa Amirul-Mu’miniin (Ali a.s), na wasiri wake, (sahaba huyu) aliyemnywesha (maji) Mtume (s.a.w.w), kisha Mtume (akamuombea dua) akasema: “ewe Mwenyezi Mungu ufanye ujana wake uwe wa muda mrefu.” Basi ilipita miaka themanini na wala hapakuonekana mvi kwenye ndevu zake wala nywele zake. Amesema Sayyidu-shuhada (a.s) katika barua aliyomuandikia Muawiyah: “Bila shaka wewe ndiye uliiyemuua Amr Ibn Al-Hamiq ambaye ni sahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), ni mja mwema ambaye alizeeka kwa ajili ya ibada, mwili wake ukakonda na rangi yake ikawa ya njano.”
Na kichwa cha sahaba huyu ndiyo kichwa cha kwanza katika Uislamu kilichochomekwa kwenye mkuki na kupelekwa kwa Muawiyah. (Taz:Tanqih Al-Maqal, Usdul-Ghabah, Al-Ghadir Juz. 11)
2. Hujur Ibn Adiyyi Al – Kindi, ni sahaba ambaye utukufu wake unajulikana mno, kiasi kwamba kalamu haiwezi kusimulia ipasavyo, naye yu miongoni mwa mashahidi waliohuru, waliohama kufuata haki na waliodhihirisha mapenzi yao kwa Amirul-Mu’miniin (Ali a.s) huyu naye aliuawa na Muawiya katika mwaka wa 51 A.H. au 53 A.H. (Taz: Tanqih Al – Maqal – Na Usdul – Ghabah).

**Source URL:**
https://www.al-islam.org/swali-la-sheikh-abdullah-saleh-al-farsy-na-jibu-la-imam-muhammad-husain-kashiful-ghitaa-wa-najaf#comment-0

**Links**

[1] https://www.al-islam.org/organization/bilal-mission-tanzania
[2] https://www.al-islam.org/printpdf/book/export/html/45917
[3] https://www.al-islam.org/printepub/book/export/html/45917
[4] https://www.al-islam.org/printmobi/book/export/html/45917
[5] https://www.al-islam.org/person/sheikh-ramadhan-idris-kwezi